Nambari ya Mtahiniwa _____

SMZ

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA

126 HISTORIA

MUDA: SAA 2.00 JUMATATU 21 DISEMBA, 2020 MCHANA

MAELEKEZO KWA WATAHINIWA

1. **Mtihani huu una sehemu TATU (3) A, B na C.**
2. **Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B. Jibu maswali MANNE (4) kutoka sehemu C.**
3. **Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
4. **Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.**
5. **Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.**
6. **Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	**ALAMA**	**SAINI**
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
11.		
JUMLA		

Mtihani huu una kurasa 8 zenye maandishi

Nambari ya Mtahiniwa _____

SEHEMU A: (Alama 20)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Chagua jawabu sahihi na uandike herufi yake katika jadweli lililopo hapo chini.

   i. Mfano wa jamii za Tanganyika zilizoishi maisha ya Ujima ni

   A. Watanga na Wamasai
   B. Wanyamwezi na Wakurya
   C. Wamasai na Wandorobo
   D. Wakurya na Wanyakyusa

   ii. Miamba migumu inayotokea baada ya mlipuko wa volcano ndio yenye uwezekano wa kuwa na

   A. Dhahabu B. Chuma C. Udongo D. Chumvi

   iii. Moja ya sifa ya utawala wa moja kwa moja

   A. Uliwashirikisha viongozi wa jadi kutawala
   B. Ulishiriki katika kuchagua viongozi wa jadi
   C. Haukuwashirikisha viongozi wa jadi kutawala
   D. Waliwaruhusu machifu kusimamia shughuli za uzalishaji

   iv. Harakati za ukombozi nchini Msumbiji ziliungwa mkono na

   A. Umoja wa Mataifa
   B. Benki ya Dunia
   C. Jumuiya ya Afrika Mashariki
   D. Shirika la kijeshi la nchi za Ulaya Magharibi

   v. Wageni wa mwanzo kuja Zanzibar walitokea

   A. Ulaya B. Ghuba ya Uajemi C. China D. Ureno

   vi. Kodi ya kichwa ilitozwa kwa wananchi wenye umri wa miaka

   A. 20 B. 25 C. 15 D. 18

   vii. Tanganyika ilipokuwa na serikali kamili tarehe 9 Disemba 1961, Waziri Mkuu alikuwa

   A. Thabit Kombo
   B. Gavana Richard
   C. Rashid Kawawa
   D. Said Natepe

   viii. Nchi ya Ghana ilipata uhuru mnamo mwaka

   A. 1959 B. 1957 C. 1954 D. 1956

ix. Historia ya kufanana ambayo Zanzibar na Tanganyika walikuwa nayo kabla ya Muungano ni

A. Walikuwa na mfumo wa vyama vingi vya siasa

B. Walikuwa na itikadi tofauti za kisiasa

C. Walitawaliwa na Mjerumani

D. Walitawaliwa na Muingereza

x. Mfanyabiashara ambae alinufaika na biashara ya utumwa alikuwa

A. Hemed bin Mohammed B. Richard Lander

C. John Speke D. Sultan Seyyid Said

JAWABU

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

2. Andika **Kweli** mbele ya maelezo sahihi au **Si kweli** mbele ya maelezo yasiyo sahihi.

i. Utaalamu wa kutengeneza na kutumia zana za chuma ulianza mwaka 100 Kabla Kristo. _____

ii. Nchi ya Kenya na Uganda zilitawaliwa kwa mfumo wa aina moja. _____

iii. Bwana Heri na Abushiri waliishi maeneo ya pwani. _____

iv. Wageni kutoka Asia walipora bidhaa za asili kama shanga, vikoi, kanzu na kofia. _____

v. Miongoni mwa sekta kuu za uchumi wa kikoloni ni biashara na viwanda. _____

Taifa la Urusi lilikuwa ni la dola ya Kijamaa. _____

vi. Jumuiya ya Washirazi ilianzishwa kama klabu ya mpira. _____

vii. Mabadiliko ya sekta ya elimu baada ya ukoloni yalizingatia mila,

viii. maadili na desturi za Waafrika. _____

ix. Wakoloni walimuweka Dkt. Kwame Nkrumah gerezani kwa tuhuma za kuchochea migomo. _____

x. Mfumo wa chama kimoja cha siasa haukuleta maendeleo yeyote Afrika. _____

Nambari ya Mtahiniwa _____

SEHEMU B: (Alama 40)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

3. Linganisha vyama vya siasa kutoka **KIFUNGU A** na kazi zao kutoka **KIFUNGU B.** Andika herufi ya jawabu ndani ya jadweli liliopo hapo chini.

KIFUNGU A	KIFUNGU B
i. ANC ii. TANU iii. AMNUT iv. UTP v. TAA	a. Kiliiomba serikali ya kikoloni kuharakisha uhuru wa Tanganyika b. Kilidai uhuru wa Watanganyika kwa kabila moja tu c. Kilianza harakati za kudai uhuru wa Tanganyika d. Kilidai uhuru wa Watanganyika wa makabila, jinsi, dini na rangi zote e. Kilipendekeza Waafrika watafute elimu ili washirikiane na wakoloni f. Kiliiomba serikali ya kikoloni kuchelewesha uhuru wa Tanganyika g. Kilidhamiria kuleta uhuru wa watu wa Afrika tu na sio wa mataifa mengine waliokuwa wakiishi Tanganyika h. Kiliundwa na wabunge walioteuliwa na gavana katika Baraza la Kutunga Sheria

JAWABU

i.	ii.	iii.	iv.	v.

4. Jaza nafasi zilizowazi kwa kuweka jibu sahihi ulilopewa kwenye mabano.

a) Waafrika walinyimwa huduma ya _____ kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar.

b) Mkutano wa Berlin uliweka _____ ya kuligawa na kulitawala Bara la Afrika.

c) Miongoni mwa mazao ya biashara yaliyolimwa wakati wa ukoloni ni _____

d) Kabila lililokuwa na nguvu zaidi kuliko wakoloni nchini Uganda ni _____

e) Changamoto za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hutatuliwa kwa njia ya

_____

(pamba, mashirikiano, Buganda, misingi, mwani, mjadala, makaazi)

5. Jibu maswali yafuatayo kwa ufupi.

   a) Unafahamu nini kuhusu "vitangulizi vya ukoloni?"

   _____

   _____

   _____

   b) Bainisha mapambo mawili (2) yaliyotengenezwa kutokana na chuma wakati wa zama za chuma.

      i. _____

      ii. _____

   c) Taja matabaka mawili (2) yaliyokuwapo katika uchumi wa kikoloni.

      i. _____

      ii. _____

   d) Toa kazi mbili (2) zinazofanywa na kiongozi wa familia kwa sasa.

      i. _____

      _____

      ii. _____

      _____

   e) Andika nchi nne (4) wanachama wa Jumuiya ya SADC.

      i. _____

      ii. _____

      iii. _____

      iv. _____

Nambari ya Mtahiniwa _____

SEHEMU C: (Alama 40)

Jibu maswali MANNE (4) tu katika sehemu hii.

6. Eleza kwa ufupi athari nne (4) zilizojitokeza baada ya kuenea kwa utaalamu wa chuma.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

7. Chambua hatua nne (4) zilizochukuliwa na nchi huru za Afrika katika kujikwamua kiuchumi.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Nambari ya Mtahiniwa _____

8. Kwa nini wakoloni walianzisha mfumo wa utawala usio wa moja kwa moja katika bara la Afrika? Toa hoja nne (4).

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

9. Fafanua namna mawasiliano na usafiri vilivyotolewa na wakoloni Afrika.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

10. Ainisha sababu nne (4) za kuingia kwa wageni Tanganyika kutoka Ulaya.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

11. Elezea mbinu nne (4) zilizotumika katika kupata uhuru wa Zimbabwe.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

==========